| | | |
|---|---|---|
| **AFRICAN UNION** | | **UNION AFRICAINE** |
| **الاتحاد الأفريقي** | | **UNIÃO AFRICANA** |
| **UMOJA WA AFRIKA** | | **UNIÓN AFRICANA** |

**Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844**
**Website:** www.au.int

**BARAZA KUU**
**Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na nne**
**15 Januari - 15 Februari 2024**
**Addis Ababa, ETHIOPIA**

**EX.CL/1455(XLIV)Rev.1**
Asili: Kiingereza

# RIPOTI YA KAMATI NDOGO YA MABORESHO YA MIUNDO

AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int

# UONGOZI WA KAMATI YA KUDUMU YA WAWAKILISHI (PRC) – KAMATI NDOGO YA MABORESHO YA MIUNDO

## RASIMU YA RIPOTI

**Tarehe 14 Desemba 2023**

**Mkutano kwa Njia ya mtandao**

## A. UTANGULIZI

1. Mkutano wa Uongozi wa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Maboresho ya Miundo ulifanyika kwa njia ya mtandao tarehe 14 Desemba 2023.

2. Mkutano huo uliongozwa na Mhe. Balozi Amma A. Twum-Amoah, Balozi wa Jamhuri ya Ghana na Mwakilishi wa Kudumu katika Umoja wa Afrika.

## B. MAHUDHURIO

3. Wajumbe wafuatao wa Uongozi walihudhuria mkutano:

Congo
Djibouti
Ghana
Morocco
Zimbabwe

## C. KUJADILI RASIMU YA AJENDA

4. Rasimu ya ajenda ya mkutano ilipitishwa kama ifuatavyo:

1. Hotuba ya Ufunguzi ya Mwenyekiti wa Kamati Ndogo
2. Kupitishwa kwa Ajenda
3. Kujadili Rasimu ya Uamuzi wa kukasimisha mamlaka ya kuidhinisha miundo
4. Mengineyo
5. Hotuba ya ufungaji

## D. HOTUBA YA UFUNGUZI

5. Katika hotuba yake ya ufunguzi, Mhe. Balozi Amma A. Twum-Amoah, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Maboresho ya Miundo ya PRC aliwakaribisha wajumbe wenzake kwenye mkutano.

6. Mwenyekiti aliwajulisha Wajumbe wa Uongozi waliohudhuria kikao hicho kuwa aliitisha kikao hicho katika ngazi ya Uongozi kutokana na taarifa zilizopokelewa na Kamisheni kwamba baada ya mashauriano ya ndani, Kamisheni iliazimia kwamba hakuna miundo itakayowasilishwa kwa ajili ya kujadiliwa katika Mkutano ujao wa Wakuu wa Nchi na Serikali. Aidha alisema kuwa Kamisheni ilibainisha kwamba mchakato wa mageuzi unaoendelea utapewa kipaumbele. Hivyo, ilipendekezwa kuwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali ukasimu mamlaka yake kwa Baraza Kuu ili kujadili miundo ya Taasisi ya Afrika ya Huduma za Kibinadamu (AHA) na Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi (AIMEC) wakati wa mkutano wake wa katikati ya 2024.

7. Kisha Mwenyekiti aliwajulisha Wajumbe wa Uongozi kwamba madhumuni ya kikao hicho ni kujadili ombi lililotolewa na Kamisheni na kutoa uamuzi kuhusu ombi hilo.

**E. KUJADILI RASIMU YA UAMUZI WA KUKASIMISHA MAMLAKA YA KUIDHINISHA MIUNDO**

8. Ufafanuzi uliombwa kutoka kwa Sekretarieti kuhusu vyombo vilivyowasilishwa ili kujadiliwa.

9. Sekretarieti ilifafanua kuwa vyombo vilivyowasilishwa havikuwa sehemu ya mchakato unaoendelea wa mageuzi kwa vile havipo.

10. Sekretarieti ilitoa ufafanuzi zaidi kwa Uongozi kwamba vyombo hivyo ni:
  i) Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi (AIMEC) (AIMEC); na
  ii) Taasisi ya Afrika ya Huduma za Kibinadamu (AHA).

11. Sekretarieti pia iliujulisha Uongozi kwamba Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu (AfCHPR) mjini Banjul, ilitaka kupendekeza maboresho ya miundo yake. Hata hivyo, baada ya mashauriano ya ndani, Kamisheni iliona kwamba mchakato wa mageuzi upewe kipaumbele.

12. Kisha Sekretarieti ilieleza kwamba haikuwa lazima kwa ombi la AfCHPR kujadiliwa, kwa vile ni sehemu ya mchakato wa mageuzi na hivyo hakutakuwa na tija ya kupitia upya miundo mipya iliyopendekezwa na Tume huko Banjul katika hatua hii.

13. Katika majibu yao, Wajumbe wa Uongozi walisema kuwa hawakuwa na pingamizi la kuahirishwa kwa mapitio ya miundo ya vyombo tajwa hapo juu hadi Julai 2024. Uongozi pia ulikubaliana na maoni yaliyotolewa na Kamisheni kuhusu pendekezo la Tume ya Banjul la uboreshaji wa muundo wake.

14. Wajumbe wa Congo walitaka kupata ufafanuzi kuhusu suala lililojadiliwa na walijulishwa na Mwenyekiti kwamba lengo la mkutano huo lilikuwa kujadili pendekezo la Kamisheni na kujadili rasimu ya Uamuzi iliyowasilishwa.

15. Uongozi uliomba ufafanuzi kutoka kwa Sekretarieti kuhusu suala la kukasimu madaraka kwa ajili ya kujadili miundo iliyotajwa hapo juu na uamuzi wa kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi (AIMEC).

16. Sekretarieti ilijibu kuwa mamlaka hayo yangekasimiwa kwa Baraza Kuu na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali. Sekretarieti pia ilipendekeza kuwa badala ya kuorodhesha vyombo ambavyo miundo yake ingejadiliwa mwaka 2024, katika rasimu ya Uamuzi, iachwe wazi. Sekretarieti ilifafanua zaidi kuwa uundwaji wa Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi ulitokana na Uamuzi Assembly/AU/Dec.856(XXXVI).

17. Katika majibu yake kwa pendekezo la Sekretarieti, Mwenyekiti na Wajumbe wa Uongozi walisema kwamba ni muhimu kutaja vyombo ambavyo miundo yake itajadiliwa wakati wa Mkutano wa Baraza Kuu katikati ya 2024 ili kuwa kama mwongozo.

18. Kutokana na ufafanuzi uliotolewa kuhusu suala la ukasimishaji wa mamlaka, Uongozi ulipendekeza rasimu ya Uamuzi iliyowasilishwa na Sekretarieti ifanyiwe marekebisho ili kuonyesha kuwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali unakasimu mamlaka yake kwa Baraza Kuu. Zaidi ya hayo, Uongozi ulisisitiza haja ya kuorodhesha taasisi ambazo miundo yake itajadiliwa katikati ya 2024.

19. Baada ya mapitio ya waraka uliowasilishwa kwa Uongozi kuhusu kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi, Mwenyekiti alibainisha kuwa Uamuzi huo ulihusu ‘Sheria’ za chombo hicho, na kutaka ufafanuzi kuhusu muundo wake.

20. Kwa kuwa hakukuwa na mwakilishi wa Wanasheria katika kikao hicho ili kutoa ufafanuzi zaidi, Sekretarieti ilipewa jukumu la kusambaza Uamuzi kuhusu Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi kwa Wajumbe wa Uongozi kwa ajili ya kujadiliwa na kuwa mwongozo zaidi wa kujumuishwa kwake katika orodha ya taasisi zitakazojadiliwa katika rasimu ya Uamuzi.

21. Hivyo, Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi kiliondolewa kwenye orodha, ikisubiriwa kusambazwa kwa Uamuzi wa kuundwa kwake. Kikao hicho kilikubaliana kuwa kituo kitajumuishwa pale tu Sekretarieti itakapowajulisha Wajumbe wa Uongozi kuhusu Uamuzi unaohusiana na kuundwa kwa chombo hicho.

22. Mwenyekiti alipendekeza kwamba pindi Uamuzi wa kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi utakapotolewa kwa Uongozi, rasimu ya Uamuzi wa kukasimu mamlaka inaweza kurekebishwa ili kukijumuisha. Kisha rasimu ya Uamuzi inaweza kusambazwa chini ya utaratibu wa kimya kimya kwa Nchi Wanachama wote kwa ajili ya kujadiliwa. Pendekezo hili lilikubaliwa na washiriki wote wa mkutano.

## F. HOTUBA YA UFUNGAJI

23. Mwenyekiti alihitimisha kwa kuwasilisha rasimu ya Uamuzi uliorekebishwa kuhusu kukasimu mamlaka kwa Wajumbe wa Uongozi na ulipitishwa na wote.

24. Mwenyekiti aliendelea kuukumbusha Uongozi kuwa Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi kitajumuishwa kwenye rasimu ya Uamuzi mara tu baada ya waraka husika wa kuundwa kwake kuwasilishwa kwa Wajumbe wa Uongozi na Sekretarieti. Vinginevyo, chombo pekee ambacho kingetajwa katika rasimu ya Uamuzi huo kitakuwa Taasisi ya Afrika ya Huduma za Kibinadamu.

## G. MENGINEYO NA KUAHIRISHA

25. Kwa kuwa hakukuwa na ombi la kujadili mambo mengineyo, mkutano uliahirishwa.

## RASIMU YA UAMUZI

**Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali,**

1. **UKIREJELEA** Ibara ya 9(2) ya Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika, ambayo inaupa mamlaka Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kukasimu mamlaka na majukumu yake yoyote kwa Chombo chochote cha Umoja wa Afrika;

2. **UNAAMUA** kukasimu mamlaka yake kwa Baraza Kuu ili kujadili na kupitisha miundo ya:
   - Taasisi ya Afrika ya Huduma za Kibinadamu
   - Kituo cha Afrika cha Ubora wa Masoko Jumuishi

   wakati wa mkutano wake wa 45 mwezi Juni/Julai 2024.

**AFRICAN UNION UNION AFRICAINE**

**African Union Common Repository** **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-01-15

# Report of the sub-committee on structural reforms

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10492

*Downloaded from African Union Common Repository*